Ser. No. EDU 195/18

# CHUO KIKUU CHA GARISSA

## MTIHANI WA MWISHO WA SEMISTA

Idara ya **Sanaa na Sayansi ya Kijamii** Shahada ya **Elimu (B.Ed-Arts)**

Semista ya **Pili 2017/2018** **KIS 220: Fasihi Simulizi katika Kiswahili**

Muda: **Saa 3** Tarehe:**10/4/2018**

Mkondo**: School Based**

**Maelekezo:** Jibu swali la **KWANZA** na maswali mengine **MATATU**
Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**

---

1. (a) Unakusudia kufanya utafiti wa nyanjani kuhusu nyimbo za jamii ya Wasomali. Eleza jinsi utakavyofuata hatua zifuatazo katika utafiti wako:

   i. Maandalizi **(Alama 5)**

   ii. Ukusanyaji wa data **(Alama 5)**

   iii. Uwasilishaji wa matokeo **(Alama 5)**

   (b) Jadili changamoto zozote TANO zinazoikabili fasihi simulizi katika jamii ya kisasa huku ukipendekeza nini kifanyike ili kusuluhisha changamoto zenyewe. **(Alama 10)**

2. (a) 'Methali hutumia lugha ya kitamathali.' Jadili kauli hii ukizingatia mifano yoyote MITANO. **(Alama 5)**

   (b) Eleza kwa mifano mwafaka mambo yoyote MATANO yanayochangia kubadilika kwa fasihi simulizi. **(Alama 10)**

3. (a) Jadili dhima zozote TANO za fanani wa fasihi simulizi katika jamii yake. **(Alama 5)**

   (b) Unakusudia kusimulia hadithi kwa hadhira ya watoto. Eleza jinsi utakavyotumia utendaji kufanikisha usimulizi wako. **(Alama 10)**

4. Soma mfano ufuatao wa majigambo kutoka katika jamii ya Wahaya kisha ujibu maswali yanayofuata: